

Taasisi zifuatazo ziko tayari kukusaidia ikiwa umeshikwa na hasara:

Bwana Uholanzi

Dutch Foundation of Religious Against Trafficking in Women

Sint Janssingel 92
NL 5211 DA Den Bosch
The Netherlands (Holland)
Tel:+31- 73 – 615 44 44
Fax: +31-73 – 615 44 49
E-mail: srtv@srtv.info
Website : www.srtv.info
Bank-Giro no 420557

Bwana Ujerumani


Solwodi (Solidarity with women in distress)

Probstei-Strasse.2
D-54154 Boppard Hirzenach,
Germany
Tel. +49-67 41 22 32
Fax: +49-67 41 23 10
E-mail: info@solwodi.de
Website : www.solwodi.de

Anwani nchini mwako unakoweza kupata msaada:



JE, ULAYA NI NCHI YA AHADI?



USIKUBALI MANENO MATAMU YOYOTE

Swahili

*Dutch Foundation of
Religious against
Trafficking in
Women*




**Je kuna mtu ye yote
aliyekuahidia kupata maisha
mazuri utakapokwenda
Ulaya?**

**Agalia !!!
Inawezekana kuna mtego hapa.**

ONYO

KWA WASICHANA NA KINAMAMA



**Kusudi la karatasi hij ni kuwaarifu
wasichaana na wakinamama katika nchi za
Afrika kuhusu hatari zilizopo
wanapokwenda Ulaya.**

KWA NINI TAARIFA HII?

Ujue kwamba wasichana na kinamama wengi walikuwa kama wewe na ndoto ya kupata maisha mazuri huko Ulaya.

GRACE: baada ya kufiwa na wazazi wake Grace alitoka kijiji cha Bakwai na alifika Accra. Alitumaini kupata kazi ili apate kulea watoto wake. Siku fulani alikutana na mtu ambaye aliimwahidia kumpatia kazi kama kusuka nywele huko Ulaya apate mshahara mzuri. Hata alimlipia nauli, pasporti na visa. Alipofika Uholanzi ndoto zake zilikwisha mara. Aidha mwajiri alishika pasi yake na akakataa kuirudisha. Alimlazimisha kufanya kazi ya umalaya ili apate pesa za nauli ya kurudi.

MAMA ALI: Mama Ali aliitikia tangazo katika gazeti ambapo kijana Mdachi alitafuta rafiki wa kalam.huko Ghana . Baada ya muda huyu rafiki alimpelekea tikiti na alimwalika kufika Ujerumani. Alipofika huko Ujerumani hakupata alivyoahidiwa, wala alivyotazamia. Ilionekana kwamba rafiki wa kalamu alikuwa mzee tena mlevi, aliyempiga mara kwa mara.

LUCY BABY: Alikuwa na rafiki wengi. Watoto wake watatu walikuwa na baba tofauti; hakuna hata mmoja aliyewajali watoto Alidhani kuwa kufanya kazi kama malaya huko Uholanzi ilikuwa bora, angalau atapata pesa kwa umalaya wake. La, mtu aliyemsaidia kufika Uholanzi alimnyima pasporti yake na pesa zake. Hakupata pesa za kupeleka nyumbani kwa mama mzazi na watoto. Mara kwa mara mwajiri alimpiga au alimlazimisha kutenda mambo kinyume ya maumbile.

WASICHANA NA WAKINAMAMA WENGI WAMEKUTA MAMBO KAMA HAYO.

UULIZE MAELEZO ZAIDI AU MSAADA KUTOKA KWA YULE ALIYEKUTOLEA KARATASI HII.

Wako wasichana na kinamama wengi wanaopata matatizo huko Ulaya. Wale walioahidiwa:

-Kazi nzuri

-Mshahara wa juu

-Ndoa na mtu tajiri

wanatumaini kupata pesa nyingi kwa muda mfupi na kupata maisha bora na kurudi kwao.kuwasaidia jamaa zao.

ILA UKWELI NI UPI?

1. Ni shida sana kupata kazi huko Ulaya. Wenye vyeti vya juu tu wanapata kazi nzuri na mshahara mkubwa. Ukikosa vyeti vya kutosha itakubakia tu kazi ya kufagia barabara kwa mshahara wa chini sana.
2. Iii kukaa katika nchi za Ulaya kwa hali ya halali inatakiwa kuwa na vibali 3: Entry permit, residence permit, workperrmit.
3. Kukosa vyeti na vibali inakulazimisha kukubali mshahara mdogo sana. Mara kwa mara huwafanya wasichana kupata pesa kwa njia ya umalaya.
4. Kuna hatari kubwa ya kupata H.I.V.na ukimwi.
5. Angalia !! Ahadi zenye maneno matamu mara nyingi hazitimiliki. Ni za uwongo.



HAKIKISHA KABLA YA KUSAFIRI, KUWA KARATASI ZOTE ZA KUSAFIRIA ZIKO HALALI.

ILA IKIWA BAADA YA KUTAADHIRISHWA KWA ONYO HILO, BADO UNAAMUA KWENDA:

1. Hakikisha kwamba majina na anwani ya wale waliokualika ni sahihi na ya kuaminika.
2. Hakikisha kutoka kwa Ubalozi wa nchi utakapokwenda kwamba mwajiri anayekuahidia kukupa kazi kweli yupo, ni halali na mwaminifu.
3. Uulize zaidi taarifa kuhusu kufanya kazi ugenini kutoka kwa taasisi maalum zinazo-shughulika na wanaofanya kazi, Hakikisha kupata msaada unaotakiwa.
4. Taari fu wajamaa wako juu ya tarehe ya kuondoka, mahali utakapokwenda anwani yako pale na majina ya wale wanaokusindikiza.
USIONDOKE KWA SIRI.

PASPORTI NI MALI YAKO !!

5. Ikiwa unashikwa na hasara umwombe mwanasheria kukuwakilisha. Dai hili ni halali na ni haki yako.
6. Nenda kwa polisi wa mahali unapopata matatizo. Ni mojawapo ya kazi ya polisi kusimamisha biashara ya wasichana na wakinamama. Hakika watakusaidia.

USIOGOPE !! USIMPATIE MTU YE YOTE PASPORTI YAKO. USIKUBALI HATA SIKU MOJA.